

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



### MAHAKAMA YA TANZANIA

#### TAARIFA KWA UMMA

Mahakama ya Tanzania inatoa taarifa kwa Umma kwamba **Jaji Mkuu wa Tanzania Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamis Juma** amefuta ada kwa nyaraka mbalimbali za kimahakama. Katika Maelekezo Namba 1. ya Jaji Mkuu ya Mwaka 2018, Mheshimiwa Jaji Mkuu ametaka nakala za hukumu, uamuzi mdogo, amri, amri itokanayo na uamuzi wa Mahakama pamoja na Tuzo za Hukuma za Mahakama zitolewe kwa wadaawa bure. Maelekezo haya yanafuta ada kwa nyaraka zilizotajwa katika ngazi za Mahakama Kuu, Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama za Wilaya, na Mahakama za Mwanzo.

Aidha Mheshimiwa Jaji Mkuu amewaelekeza Manaibu Wasajili na Mahakimu Wakazi Wafawidhi kuhakikisha kwamba wanatekeleza maelekezo haya mara moja kwa kuweka mfumo wa kufuatilia utoaji wa nyaraka hizi kwa wadaawa kwa wakati na bila malipo yoyote. Hali kadhalika, Mheshimiwa Jaji Mkuu ametoa maelekezo kwa Watendaji wa Mahakama au yeyote anayehusika na masuala ya utawala kuhakikisha anawezesha nyaraka zilizotajwa kutolewa bure na kumfikia kila mdaawa.

Wananchi wote mnatangaziwa kwamba, yeyote atakayedaiwa malipo ili kupata nyaraka hizi za Mahakama, au kuchelewa kupata uamuzi ndani ya siku 21 tokea uamuzi utolewe atoe taarifa kwa ujumbe mfupi kwenda namba **0752 500 400** au namba za simu zilizopo katika mabango yaliyobandikwa katika kuta za kila Mahakama na ofisi za Wakuu wa Wilaya na Mahakama. Kwa namba hizo mwananchi anaweza kutoa taarifa TAKUKURU au kwa uongozi wa Mahakama. Kwa malengo ya utambuzi wa mhusika, chukua namba ya kitambulisho atakachokuwa amevaa mtoa huduma atakayedai fedha kwa kutoa nyaraka zilizofutiwa ada na Mhe Jaji Mkuu. Kumbuka namba hizi za simu ni kwa ajili ya kutoa malalamiko kwa yeyote ambaye hataridhika na alivyohudumiwa na mtumishi wa Mahakama.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Katarina Revocati'.

Katarina Revocati  
**MSAJILI MKUU**  
**MAHAKAMA YA TANZANIA**  
12.03.2018